

Jipange kwa Hatua Zilizoboreshwa za Usalama za COVID

Shule za Umma za Albuquerque zinafanya kila kitu kinachowezekana ili kuwaweka wanafunzi salama na shuleni huku idadi ya visa vya COVID katika New Mexico vikisalia juu.



Shule za Umma za Albuquerque zinajua kwamba ongezeko linaloendelea la visa vya COVID-19 katika taifa nzima ni sababu ya kuwa na wasiwasi, na tunataka kukuhakikishia wilaya inafanya kila kitu kinachowezekana kuwaweka wanafunzi na wafanyakazi wetu salama, kuzuia kuenea kwa ugonjwa, kupunguza usumbufu, na cha maana zaidi, kuendelea na masomo na mafunzo ya ana kwa ana.

Timu ya APS ya kushughulikia COVID-19 inaendelea kushauriana na wataalamu wa afya. Hapa chini kuna muhtasari wa njia ya safu ya usalama ya COVID na mazingatio ya vigezo vya shule kutekeleza mikakati iliyoongezeka ya kupunguza hatari na kufungwa kwa madarasa/shule, ikihitajika. Tafadhali kumbuka vigezo vinavyopendekezwa vinahesabiwa bila kuwajumuisha wale walio shuleni wakati wa maambukizi.

- Baada ya shule kufikia kigezo cha asilimia 3 au zaidi cha idadi yake (wanafunzi na wafanyakazi) cha maambukizi katika siku 14 zilizopita, hatua zilizoboreshwa za usalama za COVID-19 zitapendekezwa. Wafanyakazi wa wilaya watatekeleza ziara ya shule, watakutana na wasimamizi wa shule ili kuhakikisha utiifu wa hatua za sasa, na kutoa mapendekezo ya mikakati iliyoboreshwa ya kupunguza hatari.
- Shule kufikia kigezo cha asilimia 3 au zaidi cha idadi yake (wanafunzi na wafanyakazi) cha maambukizi katika siku 14 zilizopita itahitaji hatua zilizoboreshwa za usalama za COVID-19. Mfanyakazi wa wilaya atatekeleza ziara ya shule, atakutana na wafanyakazi wa shule ili kuhakikisha utiifu wa hatua za sasa, na kutoa mapendekezo na kutambua mikakati iliyoboreshwa ya kupunguza hatari.
- Siku 7-14 baada ya shule kuhitajika kutekeleza hatua zilizoboreshwa za usalama za COVID-19, kiwango cha visa vya sasa vya COVID-19 kitapitiwa, na ziara ya shule ya kufuatilia itatekelezwa ili kubainisha kama mikakati ya ziada ya kupunguza hatari inafaa.
- Siku 14-21 baada ya shule kuhitajika kutekeleza hatua zilizoboreshwa za usalama za COVID-19, kiwango cha visa vya sasa vya COVID-19 kitapitiwa. Mikakati iliyoboreshwa ya kupunguza hatari itaondolewa wakati mfanyakazi wa wilaya atakapothibitisha visa vya sasa vya COVID-19 viko chini ya asilimia 3 ya idadi ya shule (wanafunzi na wafanyakazi) katika siku 14-21 zilizopita.

<https://www.aps.edu/news/news-from-2021-2022/plan-for-enhanced-covid-safe-practices>

- Viwango vya ziada vya vigezo vitazingatiwa ikihitajika ili kubainisha kufungwa kwa madarasa/shule (k.m., ukosefu wa wafanyakazi wa kutoa mgao salama wa watu wazima kwa wanafunzi, ashirio la maambukizi shuleni, au vipengele vingine husika vinavyochangia).

Mpango huu, ukichanganywa na zana zinazopatikana tayari na zinazotumika, kama vile chanjo, vipimo, vipimo vya watu waliokaribiana, kuvaa barakoa, kutotangamana na watu, na hewa safi na usafi ulioboreshwa wa mazingira, unaweza kutoa kinga bora dhidi ya virusi vinavyoenea.